



# >>> Orientation to Ontario

## HAKI NA HUDUMA ZA KISHERIA

### MKATABA WA KANADA WA HAKI NA UHURU

Mkataba unalinda haki na uhuru zifuatazo kwa wanaume na wanawake:

- Uhuru wa kushiriki imani yako.
- Uhuru wa kujumuika na mtu yeyote unayemtaka.
- Uhuru wa kufuata dini yako.
- Haki ya kuishi popote nchini Kanada.
- Haki ya kulindwa dhidi ya kukamatwa kinyume cha sheria, na haki ya kufuata utaratibu wa sheria.
- Haki ya ulinzi sawa na manufaa sawa ya sheria bila ubaguzi kwa misingi ya rangi, taifa au asili ya kabilia, rangi, dini, jinsia, umri, au ulemavu wa kiakili au kimwili.
- Haki ya kupokea huduma kutoka kwa serikali ya jimbo kwa Kiingereza au Kifaransa.

Jifunze zaidi kuhusu Mkataba katika Idara ya Haki: [canada.ca](http://canada.ca) au [findlink.at/constiacts](http://findlink.at/constiacts)

### KANUNI YA HAKI ZA BINADAMU YA ONTARIO

Chini ya Kanuni hiyo, ni kinyume cha sheria kumbagua au kumnyanyasa mtu katika maeneo ya ajira, makazi na huduma kwa misingi ya umri wa mtu, rangi, kabilia, mahali

anakotoka, dini, ulemavu, hali ya ndoa (pamoja na hali ya uwenza wa jinsia moja), utambulisho, rekodi ya makosa, jinsia au mwelekeo wa kijinsia.

Ikiwa unahisi umebaguliwa kutokana na mojawapo ya misingi hii iliyolindwa, unaweza kuwasilisha kesi kwa Mahakama ya Haki za Kibinadamu. Ili kupata usaidizi wa kisheria kutoka kwa Kituo cha Usaidizi wa Kisheria wa Haki za Kibinadamu, tembelea [hrlsc.on.ca](http://hrlsc.on.ca)

Jifunze zaidi kuhusu haki za binadamu huko Ontario katika Tume ya Haki za Kibinadamu ya Ontario: [ohrc.on.ca](http://ohrc.on.ca)

### HAKI ZA VIJANA

Ingawa kijana anachukuliwa kuwa mtu mzima katika umri wa miaka 18, kuna sheria nydingine kulingana na umri. Huko Ontario, lazima uwe na umri wa miaka 19 ili kunywa au kununua bidhaa za tumbaku. Umri wa idhini ya kufanya ngono ni miaka 16, isipokuwa kwa baadhi.

Pata maelezo zaidi kuhusu umri wa idhini katika [justice.gc.ca](http://justice.gc.ca) au [findlink.at/ageconsent](http://findlink.at/ageconsent).

### HUDUMA ZA KISHERIA

Pata maelezo zaidi kuhusu mfumo wa kisheria wa Ontario na jinsi ya kufikia huduma za kisheria:

Kwa saraka ya mawakili na wasaidizi wa kisheria Ontario, tembelea Shirika la Wanasheria la Upper Kanada katika [ontario.ca](http://ontario.ca)

Funded by / Financé par

Msaada wa Kisheria Ontario hutoa huduma za kisheria kwa watu walio na mapato ya chini. Piga simu [1-800-668-8258](tel:1-800-668-8258) au tembelea [legalaid.on.ca](http://legalaid.on.ca)

Settlement.org hutoa taarifa kuhusu mfumo wa kisheria wa Kanada na huduma za kisheria: [settlement.org](http://settlement.org) au [findlink.at/Legal-Serv](http://findlink.at/Legal-Serv)

Elimu ya Kisheria kwa Jamii Ontario huunda taarifa za ukweli ili kuwasaidia watu kuelewa haki na wajibu wao wa kisheria. Kwa habari zaidi, tembelea [cleo.on.ca](http://cleo.on.ca)

Kwa maelezo ya kisheria (yanapatikana katika zaidi ya lugha 170), piga simu kwa [1-866-252-0104](tel:1-866-252-0104) au tembelea Justice Ontario: [attorneygeneral.jus.gov.on.ca](http://attorneygeneral.jus.gov.on.ca)

Iwapo unaona kuwa umetendewa isivyo haki na serikali ya Ontario, unaweza kuripti tukio hilo kwa Mtetezi wa Umma wa Ontario: [ombudsman.on.ca](http://ombudsman.on.ca).

#### MAELEZO MUHIMU

Huko Ontario, sheria mbili muhimu zinalinda haki zako za kisheria na uhuru:

- **Mkataba wa Haki na Uhuru wa Kanada.**
- **Kanuni ya Haki za Kibinadamu ya Ontario**

